

GAZETI LA SERIKALI NA. 448B la tarehe 30/6/2023

SHERIA YA MIFUMO YA MALIPO,
(SURA YA 437)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 46A (2))

KANUNI ZA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA KIELEKTRONIKI YA
KUTOA FEDHA TASLIMU, 2023

MPANGILIO WA KANUNI

Kanuni *Kichwa*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UKUSANYAJI WA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA KIELEKTRONIKI
YA KUTOA FEDHA TASLIMU

4. Chanzo cha tozo.
5. Wajibu wa mkusanyaji.
6. Muda na namna ya kuwasilisha ritani.
7. Kuweka fedha zilizokusanywa kama tozo.

SEHEMU YA TATU
UFUATILIAJI WA MIAMALA YA FEDHA YA KIELEKTRONIKI

8. Ufuatiliaji.
9. Kufichua taarifa.
10. Rufaa.
11. Mamlaka ya kubadili au kurekebisha Jedwali.
12. Kufutwa.

JEDWALI

GAZETI LA SERIKALI NA. 448B la tarehe 30/6/2023

SHERIA YA MIFUMO YA MALIPO,
(SURA YA 437)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 46A (2))

**KANUNI ZA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA KIELEKTRONIKI YA
KUTOA FEDHA TASLIMU, 2023**

**SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI**

- | | |
|---|--|
| Jina na tarehe
ya kuanza
kutumika | 1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Tozo ya Miamala ya Fedha ya Kielektroniki ya Kutoa Fedha Taslimu, 2023 na zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2023. |
| Matumizi | 2. Kanuni hizi zitatumika kwa miamala yote ya fedha ya kielektroniki ya kutoa fedha taslimu inayopitia mfumo wa malipo iliyopewa leseni chini ya Sheria. |
| Tafsiri | 3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo- |
| Sura ya 437 | “Sheria” maana yake ni Sheria ya Mifumo ya Malipo; |
| Sura ya 399 | “Mamlaka” maana yake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania; |
| | “Benki” maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania; |
| | “mkusanyaji” maana yake ni benki, taasisi ya fedha au mtu aliyepewa leseni kwa ajili ya kuendesha mfumo wa kutuma na kupokea pesa kwa njia ya simu; |
| | “Kamishna Mkuu” maana yake ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka; |
| | “miamala ya fedha za kielektroniki ya kutoa fedha taslimu” maana yake ni miamala inayomuwezesha mtumiaji kutoa fedha taslimu kielektroniki; |
| | “tozo” maana yake ni tozo inayotozwa katika miamala ya kutoa fedha taslimu kielektroniki iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 46A cha Sheria; |
| | “Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha; |
| | “mtumiaji” maana yake ni mtu anayetoa fedha kielektroniki au |

dirishani isipokuwa Serikali, mfanyabiashara au biashara;
“kutoa fedha” maana yake ni kutoa fedha taslimu kutoka katika akaunti ya simu au akaunti ya benki ya mtumiaji kupitia kwa wakala, mashine za kutolea fedha taslimu au kaunta ya benki yakutolea fedha taslimu.

SEHEMU YA PILI
UKUSANYAJI WA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA
KIELEKTRONIKI YA KUTOA FEDHA TASLIMU

Chanzo cha tozo

4.-(1) Kwa mujibu wa kifungu cha 46A cha Sheria, chanzo cha tozo kitakuwa ni miamala ya fedha ya kielektroniki ya kutoa fedha taslimu inayofanywa na mtumiaji kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Tozo haitakuwa ni sehemu ya malipo au sehemu ya muamala unaohusishwa chini ya Kanuni hizi.

Wajibu wa mkusanyaji

5.-(1) Mkusanyaji atakusanya kutoka kwa mtumiaji, tozo katika kiwango kilichoainishwa katika Jedwali na kukiwasilisha kwenye Mamlaka ndani ya siku saba za mwezi unaofuata mwezi ambao tozo hiyo inahusika.

(2) Mkusanyaji atakayeshindwa kuwasilisha tozo ndani ya muda ulioainishwa, atawajibika kulipa riba kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi ambao ataendelea kutolipa tozo itakayokokotolewa kwa kiwango kitakachoainishwa na Benki.

Muda na namna ya kuwasilisha ritani

6.-(1) Mkusanyaji atawasilisha kwa Mamlaka ritani ya kipindi husika ndani ya siku saba za mwezi unaofuata mwezi ambao tozo inahusika katika namna na fomu iliyoidhinishwa na Mamlaka.

(2) Kipindi husika kitakuwa ni mwezi ambao tozo inahusika isipokuwa kama kipindi kingine kitaamuliwa na Mamlaka kwa notisi ya maandishi.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mkusanyaji anaweza kuomba Mamlaka nyongeza ya muda wa kuwasilisha ritani pale ambapo kuna sababu za msingi za kutoa nyongeza ya muda:

Isipokuwa kwamba, nyongeza ya muda iliyotolewa chini kanuni ndogo hii, haitazidi siku saba.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (3), nyongeza ya muda iliyotolewa haitaondoa wajibu wa kuwasilisha tozo.

(5) Mkusanyaji atakayeshindwa kuwasilisha ritani ndani ya muda ulioainishwa atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni moja kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi ambao ataendelea

kutowasilisha ritani.

Kuweka
fedha
zilizokusany
wa kama
tozo

7.-(1) Mamlaka itawezesha fedha zote zilizokusanywa kama tozo chini ya Kanuni hizi kuwekwa katika Mfuko Mkuu.

(2) Bila kujali ujumla wa kanuni ndogo ya (1), endapo tozo imekusanywa Tanzania Bara na tozo hiyo inahusisha miamala ya fedha ya kielektroniki iliyofanyika Zanzibar, Mkusanyaji atawasilisha tozo hiyo kwa Bodi ya Mapato Zanzibar ndani ya siku saba katika mwezi unaofuata baada ya tozo hiyo kukusanywa.

SEHEMU YA TATU
UFUATILIAJI WA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA
KIELEKTRONIKI YA KUTOA FEDHA TASLIMU

Ufuatiliaji

8.-(1) Kwa madhumuni ya ufuatiliaji wa miamala ambayo inahusu tozo, Mamlaka itaweka mfumo wa ufuatiliaji wa miamala ya kielektroniki.

(2) Bila kujali ujumla wa kanuni ndogo ya (1),
Mamlaka-

- (a) itathibitisha ritani za mkusanyaji;
- (b) itafanya ukaguzi katika eneo la mkusanyaji ili kuhakikisha Kanuni hizi zinazingatiwa;
- (c) itaomba data au taarifa yoyote kutoka kwa mkusanyaji kwa mujibu wa Kanuni hizi; na
- (d) itachukua hatua dhidi ya kutozingatiwa kwa Kanuni hizi.

(3) Data au taarifa zitakazoombwa chini ya Kanuni hizi itatolewa na mkusanyaji ndani ya siku kumi na nne.

(4) Mkusanyaji atakayeshindwa kuwasilisha data au taarifa ndani ya muda ulioainishwa bila sababu ya msingi, atawajibika kulipa faini ya shilingi laki tano kwa kila siku ambayo ataendelea kutowasilisha data au taarifa hizo.

Kufichua
taarifa

9.-(1) Mamlaka au mtu yeyote aliyeajiriwa na Mamlaka hatafichua taarifa yoyote aliyopokea au aliyopata wakati wa utekelezaji wa mamlaka au majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

(2) Kanuni ndogo ya (1) haitatumika endapo taarifa inaombwa-

- (a) na taasisi ya utekelezaji wa sheria, mahakama au mabaraza yaliyoundwa kisheria; au
- (b) kwa madhumuni ya usalama wa nchi.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni hii, mtu yeyote aliyeidhinishwa anayetekeleza au kusaidia kutekeleza maelekezo

na akafahamu taarifa yoyote, anaweza-

- (a) kufichua taarifa hiyo kwa afisa mwingine wa utekelezaji wa sheria kwa kiwango ambacho kufichuliwa huko ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya kiofisi ya mtu aliyeidhinishwa au afisa anayetekeleza sheria anayefichuliwa taarifa husika; au
- (b) kutumia taarifa hiyo kwa kiwango ambacho ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya kiofisi.

Rufaa

10. Mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza, ndani ya siku thelathini, kutaka rufaa kwa Waziri.

Mamlaka ya kubadili au kurekebisha Jedwali

11. Waziri anaweza kurekebisha au kubadili kiasi kinacholingana na viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi:

Isipokuwa kwamba, marekebisho au mabadiliko hayo hayatazidi viwango mbalimbali vilivyoainishwa katika Sheria.

Kufutwa TS. Na. 4780 la 2022

12. Kanuni za Tozo za Miamala ya Kielektroniki ya Fedha ya Kielektroniki, 2022 zimefutwa.

JEDWALI

(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)

KIWANGO CHA MALIPO YA TOZO YA MIAMALA YA FEDHA YA KIELEKTRONIKI YA KUTOA FEDHA TASLIMU

Na.	Kiwango cha Miamala ya fedha ya kielektroniki kwa shilingi	Shilingi
1.	100 hadi 2,999	10
2.	3,000 hadi 3,999	14
3.	4,000 hadi 4,999	27
4.	5,000 hadi 6,999	54
5.	7,000 hadi 9,999	56
6.	10,000 hadi 14,999	102
7.	15,000 hadi 19,999	195
8.	20,000 hadi 29,999	306
9.	30,000 hadi 39,999	351
10.	40,000 hadi 49,999	419
11.	50,000 hadi 99,999	573
12.	100,000 hadi 199,999	707

13.	200,000 hadi 299,999	821
14.	300,000 hadi 399,999	838
15.	400,000 hadi 499,999	982
16.	500,000 hadi 599,999	1245
17.	600,000 hadi 699,999	1532
18.	700,000 hadi 799,999	1700
19.	800,000 hadi 899,999	1750
20.	900,000 hadi 1,000,000	1776
21.	1,000,001 hadi 3,000,000	1875
22.	3,000,001 na kuendelea	2000

Dodoma,
30 Juni, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
Minister for Finance and Planning